MKATABA WA GLOBAL GREENS

MKATABA WA GLOBAL GREENS

Kama ilivyoidhinishwa mjini Canberra mwaka wa 2001 na kusasishwa mijini Dakar 2012 na Liverpool 2017

Global Greens ni muungano wa kimataifa wa vyama na harakati za kisiasa vya Kijani

Yaliyomo

Utangulizi 2

Kanuni 3

Hekima ya Kiikolojia 3

Haki kwa Jamii 4

Demokrasia Shirikishi 4

Kuasi Vurugu 5

Uendelevu 6

Kuheshimu Utofauti 7

Harakati za Kisiasa 8

1. Demokrasia 8

2. Usawa 9

3. Mabadiliko ya hali ya hewa na Nishati 10

4. Bioanuwai 12

5. Kuongoza utandawazi wa uchumi kwa kanuni endelevu 13

6. Haki za binadamu 14

7. Vyakula na Maji 16

8. Mipango Endelevu 18

9. Amani na Usalama 19

10. Utendakazi wa Kimataifa 20

MKATABA WA GLOBAL GREENS

Utangulizi

Sisi, kama raia wa dunia na wanachama wa Global Greens,

Kuungana katika ufahamu wetu kwamba tunategemea ubora, utofauti na maandhari mazuri ya ulimwengu, na kwamba ni jukumu letu kuyapitisha haya kama yalivyo, au yakiwa bora zaidi, kwa kizazi kijacho.

Kugundua kwamba mifumo mingi ya uzalishaji na matumizi ya binadamu kwa kuzingatia mienendo ya ukuaji wa uchumi kwa gharama yoyote ile, na utumiaji mbaya wa mali asili bila kuzingatia uwezo wa uzalishaji wa dunia, unasababisha kuzorota kwa mazingira na kupotea wa viumbe vingine vya dunia.

Kutambua kwamba ukosefu wa haki, ubaguzi wa rangi, umasikini, ujinga, ufisadi, uhalifu na vurugu, vita vya silaha na utaftaji wa faida ya haraka ni kusababisha kuenea kwa mateso ya wanadamu

Kukubali kwamba kupitia harakati zao za malengo ya kiuchumi na kisiasa, nchi zilizoendelea zimechangia uharibifu wa mazingira na hadhi za binadamu

Kuelewa kuwa watu na mataifa mengi ya ulimwengu yamekuwa masikini kwa ajili ya karne nyingi za ukoloni na unyonyaji, na hivyo kusababisha mataifa tajiri kuwa na deni la ikolojia dhidi ya mataifa yalioathiriwa na umaskini

Kujitolea kufunga pengo kati ya matajiri na masikini na kujenga uraia unaozingatia haki sawa kwa watu wote katika nyanja zote za maisha ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni

Kugundua kuwa bila usawa kati ya wanaume na wanawake, hakuna demokrasia ya kweli inayoweza kupatikana

Kujali utu wa ubinadamu na thamani ya urithi wa utamaduni

Kutambua haki za watu asilia na mchango wao katika maisha ya kawaida, na haki ya jamii zilizo na watu wachache, watu waliokandamizwa na tamaduni zao, dini, uchumi na maisha kwa ujumla.

Kuamini kwamba ushirikiano badala ya ushindani ni dhahiri kwa kuhakikisha dhamana ya haki za binadamu kama chakula bora, makazi mwafaka, afya bora, elimu, kazi ya haki, uhuru wa kujieleza, hewa safi, maji safi ya matumizi na mazingira nadhifu

Kutambua kuwa mazingira hayajui mipaka kati ya nchi

na

MKATABA WA GLOBAL GREENS

Kuendeleza juu ya Azimio la Mkusanyiko wa Kijani huko Rio mwaka wa 1992

Sisitiza umuhimu wa mabadiliko ya msingi katika mitazamo, maadili, na njia za ukuzaji na kuishi kwa watu

Kutangaza kwamba milenia mpya inatoa nafasi ya kipekee ya kuanza mabadiliko hayo

Kukata kauli kukuza dhana kamili ya uendelevu ambayo

● inalinda na kurejesha uadilifu wa mifumo ya mazingira ya dunia kwa kutilia maanani bianuwai na michakato ya asili inayohimili maisha

● inatambua uhusiano wa michakato yote ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi

● inasawazisha masilahi ya watu binafsi na ya watu wengine kwa ujumla

● inalinganisha na kuunganya uhuru na uwajibikaji

● inakaribisha utofauti ndani ya umoja

● Inapatanisha malengo ya muda mfupi na yale ya muda mrefu

● inahakikisha vizazi vijavyo vina haki sawa na kizazi cha sasa kwa faida za asili na za kitamaduni

Thibitisha jukumu letu kwa wenzetu, kwa jamii yote ya viumbe hai kwa ujumla, na kwa vizazi vijavyo

Kujitolea kama vyama na harakati za kisiasa za Kijani kutoka ulimwenguni kote kutekeleza kanuni hizi na kuunda ushirikiano wa kimataifa katika kusaidia kuzitimiza.

Kanuni

Sera za Global Greens zimetungwa kwa kuzingatia msingi wa kanuni za

Hekima ya Kiikolojia

Tunatambua kwamba wanadamu ni mojawapo ya sehemu ya ulimwengu wa asili na tunaheshimu maadili maalum ya kila aina ya viumbe hai, ikiwemo spishi zisizo za kibinadamu.

Tunatambua hekima ya watu asilia wa ulimwengu kama walezi wa ardhi na rasilimali zake.

Tunatambua kwamba jamii ya wanadamu inategemea rasilimali za mazingira ya sayari na lazima tuhakikishe uadilifu wa mazingira na kuhifadhi bianuwai na ustahimili wa mifumo inayokidhi maisha.

MKATABA WA GLOBAL GREENS

Hii inahitaji

● tujifunze kuishi ndani ya mipaka ya kiikolojia na rasilimali ya sayari

● tulinde maisha wa wanyama na mimea, na uhai vilevile ambao unakidhiwa na vitu vya asili: ardhi, maji, hewa na jua

● ambapo maarifa ni kidogo, tuchukue mwenendo wa tahadhari ili kuhakikisha kuwepo kwa rasilimali za sayari za kutosha matumizi ya vizazi vha sasa na vijavyo.

Haki kwa Jamii

Tunasisitiza kwamba mwanzo wa haki kwa kijamii ni ugawaji sawa wa rasilimali za kijamii na asili, nyumbani na kimataifa, ili kukidhi mahitaji ya kimsingi ya kibinadamu bila masharti, na kuhakikisha kuwa raia wote wanapata fursa kamilifu za kujiendeleza kibinafsi na kijamii.

Tunatangaza kuwa hakuna haki ya kijamii bila haki ya mazingira, na hakuna haki ya mazingira bila haki ya kijamii.

Hii inahitaji

● mpangilio wa haki wa dunia na uchumi dhabiti wa ulimwengu ambao utafunga pengo kubwa lililoko kati ya matajiri na masikini, ndani na kati ya nchi tofauti; kusawazisha mgao wa rasilimali tokea Kusini hadi Kaskazini; na kuziondolea nchi masikini mzigo wa madeni ambao huzuia maendeleo yao.

● kutokomeza umaskini, kama jambo la lazima kijamii, kiuchumi, na kiikolojia

● kutokomeza kutokujua kusoma na kuandika

● Dira mapya ya uraia uliojengwa kwa kuzingatia haki sawa kwa kila mtu bila kujali jinsia, rangi, umri, dini, tabaka, kabila au asili ya kitaifa, mwelekeo wa kijinsia, ulemavu, utajiri au afya

Demokrasia Shirikishi

Tunajitahidi kuwa na demokrasia ambayo raia wote wana haki ya kuelezea maoni yao, na wana uwezo wa kushiriki moja kwa moja katika maamuzi ya mazingira, kiuchumi, kijamii na kisiasa ambayo yanaathiri maisha yao; ili nguvu na uwajibikaji ziimarishwe katika jamii kwa mitaa na kanda, na kugatuliwa tu kwa viwango vya juu vya utawala wakati ambapo ni muhimu au lazima.

Hii inahitaji

● uwezeshaji wa kibinafsi kupitia upatikanaji wa taarifa zote muhimu zinazohitajika ili kufanya maamuzi yeyote, na elimu kusambazwa kote ili kuwawezesha watu wote kushiriki

● kutupilia mbali vizuizi vinavyosababishwa na mali na ubabe vinazozuia kushiriki kwa watu wengine

● Kuunda taasisi za mashinani ambazo zinawezesha maamuzi kufanywa moja kwa moja katika kiwango kifaacho na wale walioathiriwa, kwa kuzingatia mifumo ambayo inahimiza kushiriki kwa raia, hatua za hiari na uwajibikaji wa jamii

● mpango thabiti wa kuwapa vijana sauti kwa kuwaelimisha, kuwahimiza na kuwasaidia kushiriki kila nyanja ya kisiasa ikiwemo pia ushiriki wao katika taasisi zote za maamuzi.

● wawakilishi wote waliochaguliwa wamejitolea kwa misingi ya uwazi, ukweli na uwajibikaji katika utawala.

● mifumo yote ya uchaguzi ni wazi na ya kidemokrasia, na kwamba hii inasimamiwa na sheria

● katika mifumo yote ya uchaguzi kila mmoja aliyehitimu umri wa utu uzima ana kura sawa

● mifumo yote ya uchaguzi inategemea uwakilishi wa idadi kwa usawia, na chaguzi zote zinafadhiliwa na umma na kunayo mipaka madhubuti, na uwazi kamili wa michango ya mashirika na ya kibinafsi.

● kwamba raia wote wana haki ya kuwa mwanachama wa chama cha siasa cha chaguo lao katika mfumo wa vyama vingi

Kuasi Vurugu

Tunatangaza dhamira yetu ya kukataa vurugu na kujitahidi kuendeleza utamaduni wa amani na ushirikiano kati ya mataifa, ndani ya jamii na kati ya watu binafsi, kama msingi wa kuimarisha usalama ulimwenguni.

Tunaamini kuwa usalama haupaswi kuweko kwa ajili ya nguvu za kijeshi bali kwa ushirikiano, maendeleo ya kiuchumi na kijamii, usalama wa mazingira, na heshima kwa haki za binadamu.

Hii inahitaji

● dhana kamili ya usalama wa ulimwengu unaopea kipaumbele nyanja za kijamii, kiuchumi, kiikolojia, kisaikolojia na kitamaduni kwa maswala ya migogoro, badala ya dhana zitegemeazo kimsingi nguvu za jeshi kuleta amani

● mfumo wa kina wa usalama wa ulimwengu wenye uwezo wa kuzuia, kudhibiti na kusuluhisha mizozo

● kuangamiza vyanzo vya vita kwa kuelewa na kuheshimu tamaduni zingine, kutokomeza ubaguzi wa rangi, kukuza uhuru na demokrasia, na kumaliza umaskini wa ulimwenguni

● kufuatilia na kuhakikisha silaha zimeondolewa ikiwemo kwa kutumia mikataba ya kimataifa ili kuhakikisha marufuku kamili na dhahiri dhidi ya silaha za kinyuklia, kibaiolojia na za kemikali, za migodi na silaha za urani.

● Kuimarisha Umoja wa Mataifa (UN) kama shirika la kimataifa la udhibiti wa migogoro na kulinda amani

● kuweka ankufuata kanuni kali haswa kwa shughuli inayohusu usafirishaji wa silaha zinapokwenda nchi ambazo haki za binadamu zinakiukwa.

Uendelevu

Tunatambua upeo mdogo wa upanuzi wa nyenzo za jamii ya binadamu ulimwenguni, na hitaji la kudumisha bianuwai kwa njia ya matumizi endelevu ya rasilimali mbadala na utumizi wa kuwajibika wa rasilimali zisizo mbadala.

Tunaamini kuwa ili kufanikisha uendelevu, na ili kutosheleza mahitaji ya vizazi vya sasa na vijavyo katika rasilimali pungufu za ulimwengu, ukuaji unaoendelea katika utumiaji kimataifa, idadi ya watu na utofauti wa nyenzo lazima usitishwe.

Tunatambua kuwa uendelevu hautawezekana wakati umaskini unakithiri.

Hii inahitaji-

● kuhakikisha kuwa matajiri wanajipima kwa matumizi yao ili kuwaruhusu maskini sehemu yao ya haki ya rasilimali za dunia

● kufafanua upya kigezo cha utajiri ili kizingatie ubora wa maisha badala ya uwezo wa utumiaji wa kupindukia

● kuunda uchumi wa ulimwengu ambao unakusudia kukidhi mahitaji ya wote, sio tama ya wachache; na unaowezesha wale waliopo sasa kukidhi mahitaji yao, bila kuhatarisha uwezo wa vizazi vijavyo kukidhi mahitaji yao

● kuondoa sababu za ukuaji wa idadi ya watu kwa kuhakikisha usalama wa kiuchumi, na kuimarisha upatikanaji wa elimu ya kimsingi na afya, kwa wote; itakayowapa wanaume na wanawake udhibiti mkubwa juu ya uzazi wao

● Kufafanua upya majukumu na matarajioya mashirika ya kimataifa ili kupiga jeki kanuni za maendeleo endelevu

● kutekeleza mifumo ya kutoza ushuru, na vile vile kudhibiti, mfumo wa kubahatisha wa mtiririko wa kifedha

● kuhakikisha kuwa bei ya bidhaa na huduma sokoni zinajumuisha kikamilifu gharama za kimazingira ya uzalishaji na matumizi yao

● kufikia utumiaji nadhifu wa rasilimali na nishati na uvumbuzi na utumiaji wa teknolojia endelevu kimazingira

● kuhimiza kujitegemea kwa kiwango kikubwa iwezekanavyo ili kuunda jamii zenye dhamana na za kuridhisha

● kutambua umuhimu wa tamaduni na mienendo ya vijana na kuhimiza maadili ya uendelevu ndani ya tamaduni hiyo.

Kuheshimu Utofauti

Tunaheshimu utofauti wa kitamaduni, lugha, kabila, kijinsia, kidini na kiroho ndani ya muktadha wa jukumu la kila mmoja wetu kwa viumbe vyote.

Tunatetea haki ya watu wote, bila ubaguzi, kwa mazingira yanayostawisha utu wao, afya ya mwili, na ustawi wa kiroho

Tunakuza uendelezaji wa uhusiano wenye heshima, uhusiano mzuri na wa uwajibikaji kwa pande zote za mgawanyiko kwa ustawi wa jamii ya tamaduni mbalimbali.

Hii inahitaji

● Kutambua haki za watu asilia kwa njia za msingi za maisha yao, kiuchumi na kitamaduni, pamoja na haki za ardhi na kujiamulia; na kutambua mchango wao katika urithi wa utamaduni wa kitaifa na ulimwengu mzima.

● utambuzi wa haki za kabila za watu walio wachache wa kukuza utamaduni, dini na lugha bila ubaguzi, na kushiriki kikamilifu kisheria, kijamii na kitamaduni katika mchakato wa demokrasia.

● Kutambua na kuheshimu uchache wa kijinsia

● Usawa kati ya wanawake na wanaume katika nyanja zote za maisha ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni

● ushiriki mkubwa wa tamaduni ya vijana kama mchango muhimu kwa maono yetu ya Kijani, na kutambua kuwa vijana wana mahitaji tofauti pamoja na njia zao kujieleza.

Harakati za Kisiasa

1. Demokrasia

1.0 Watu wengi wa ulimwengu wanaishi katika nchi zilizo na serikali zisizo na demokrasia ambapo ufisadi umeenea na ukiukkaji wa haki za binadamu na udhibiti wa vyombo vya habari ni kawaida. Demokrasia zilizoendelea zinakabiliwa na aina zisizo wazi za ufisadi kupitia umiliki wa vyombo vya habari, ufadhili wa kisiasa na mashirika, utaratibu wa kutengwa wa kijamii, kikabila, kitaifa na kidini, na mifumo ya uchaguzi ambayo inabagua maoni mbadala na vyama vipya na vidogo.

Wanakijani -

1.1. Wanao, kwa kipaumbele, himizo na uungwaji mkono wa harakati za mashinani na mashirika mengine ya asasi za kiraia zinazofanya kazi ya kuhimiza demokrasia, uwazi na uwajibikaji katika kila ngazi za serikali.

1.2 Wanaunga mkono kikamilifu kuwapa vijana sauti kupitia kuelimisha, kutia moyo na kusaidia ushiriki wa vijana katika kila nyanja ya hatua za kisiasa.

1.3 Watajitahidi kuleta demokrasia kwa uhusiano wa kijinsia kwa kukuza upatanishi unaofaa ili kuwawezesha wanawake na wanaume kwa usawa kushiriki katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijamii.

1.4 Wanaunga mkono mkutano wa Shirika la Ushirikiano wa Kichumi na Maendeleo (OECD) juu ya kupambana dhidi ya Utoaji Rushwa kwa Maafisa wa Umma wa Kigeni katika Biashara ya Kimataifa na wanayahimiza mashirika ambayo hayajajiunga kutia saini na kuridhia bila kupoteza muda zaidi.

1.5 Wanazingatia haki ya wananchi kupata habari rasmi na uhuru na kujisimamia kwa vyombo vya habari.

1.6 Watafanya juhudi kwa minajili ya ufikiaji wa ulimwengu kwa mawasiliano ya elektroniki na teknolojia ya habari, kama kigezo cha chini, kupitia redio, mtandao wa kijamii na barua pepe. Tutafanya juhudi pia kupata teknolojia hizi kwa bei rahisi iwezekanavyo.

1.7 Wanahimiza mfumo wa kisheria wa kidunia ambao unahakikisha haki ya kujitetea na kuhakikisha kuwepo kwa uwiano kati ya makosa na adhabu.

1.8 Wanaunga mkono ufadhili wa umma wa uchaguzi, na hatua za kuhakikisha michango yote ni wazi na inawajibika na haina ushawishi usiofaa kwa njia yeyote ile.

1.9 Watapinga utawala wa serikali wa ushirika, haswa ambapo raia wananyimwa haki yao ya kushiriki kisiasa.

1.10 Wanaunga mkono mgawanyoo wa mamlaka kati ya serikali, mifumo ya kisheria na mahakama, na mgawanyo wa serikali na dini.

1.11 Wanaunga mkono maendeleo na uimarishaji wa serikali za mashinani.

1.12 Wanaunga mkono urekebishaji wa taasisi za serikali ili kuimarisha demokrasia na kuzifanya ziwe na uwazi na ufanisi katika kutimiza lengo la nguvu za raia na maendeleo endelevu.

1.13 Wanaunga mkono uboreshaji wa utawala wa taasisi za kimataifa za ulimwengu kwa kuzingatia misingi sahihi ya kidemokrasia kwa wote.

2. Usawa

2.0 Tofauti za viwango vya maisha na nafasi za kujiendeleza ulimwenguni siku hizi hazikubaliki. Deni la mataifa maskini la trilioni 3.7, dollar za Kimarekani, ni juu zaidi kuliko wakati mwingine wowote, wakati nchi za Shirika la Ushirikiano wa Kichumi na Maendeleo (OECD) zinatoa asilimia 0.31 tu ya pato la kitaifa katika misaada. Asilimia 20 ya watu walio tajiri zaidi ulimwenguni wana 83% ya mapato ya ulimwengu wakati 20% walio maskini zaidi, ikiwemo vijana asilimia 50, wamegawana 1% pekee ya mapato haya na watu bilioni 2.6 wanajikidhi kwa chini ya dola 2 za Kimarekani kwa siku. Asilimia 60 ya watu maskini zaidi duniani ni wanawake. Watoto milioni 130 hawaendi shuleni na watu wazima milioni 800 hawawezi kusoma wala kuandika, theluthi mbili kati yao ikiwa ni wanawake. Ukuaji wa idadi ya watu umepungua lakini idadi ya watu ulimwenguni inakadiriwa kuongezeka kutoka bilioni 6.1 mwaka wa 2000 hadi bilioni 8.9 mwaka 2050, ongezeko la 47%. Virusi vya Ukosefu wa kinga kwa binadamu (HIV) na ugonjwa wa kifua kikuu (TB) vimebakia kuwa shida kubwa sana.

Wanakijani -

2.1 Watafanya juhudi kuongeza misaada ya serikali kwa nchi zinazoendelea, na kuunga mkono usaidizi kuelekezwa kwa walio maskini zaidi, vipaumbele vikidhamiriwa kwa kufanya kazi na jamii mashinani.

2.2 Watafanya bidii kuboresha haki, hadhi, elimu na ushiriki wa kisiasa kwa wanawake.

2.3 Tunajitolea kwa lengo la kuwezesha kila mtu kupata elimu ya hali ya juu ya shule ya msingi ulimwenguni kote ifikapo mwaka 2015, ikifadhiliwa kupitia kuongezeka kwa misaada na kutupilia deni zingine.

2.4 Watafanya juhudi ili kufutiliwe mbali madeni ya nchi zinayoendelea haswa ya nchi masikini zaidi, na kuunga mkono utumiaji wa dhamana ya kuhakikisha kuwa akiba kutoka kwa ufutaji wa madeni inaelekezwa kwa upunguzaji wa umaskini na uhifadhi wa mazingira, na kwamba michakato ya uwazi na ya uwajibikaji inafwatwa kukiwa na ushirikishi kamili wa jamii zinazohusika.

2.5 Wanazingatia hatua za pamoja za kupambana na maradhi enevu, Ukimwi, Kifua Kikuu na ugonjwa wa malaria zikiwa kipaumbele, haswa barani Afrika, ambapo juhudi maradufu zinahitajika kufanikisha ufikiaji wa watu wote kwa matibabu ya bei nafuu, na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi, haswa kupitia elimu.

2.6 Twatambua haki ya fidia ya watu wanaopoteza uwezo wa kutumia rasilimali zao kwa ajili yakufurushwa na sababu za uharibifu wa mazingira au sababu zinazosababishwa na binadamu kama ukoloni na uhamiaji.

2.7 Watatathmini uhusiano kati ya umiliki wa kipekee wa mali na matumizi ya kipekee ya rasilimali zake, kwa lengo la kupambana na matumizi mabaya ya mazingira na kupanua uwezo wa watu zaidi kuitumia ili kuimarisha maisha ya msingi kwa wote, haswa kwa jamii asili.

2.8 Tutafanya juhudi kuhakikisha kuwa wanaume, wanawake na watoto wanaweza kufikia usalama wa kiuchumi, bila hatari ya shughuli zinazoweza kuharibu sifa na hadhi binafsi kama vile ponografia, ukahaba au uuzaji wa viungo vya ndani vya mwili.

2.9 Tutajitolea kushughulikia ugawaji sawa wa ustawi na kuunda fursa sawa ndani ya jamii zetu zote, tukitambua kuwa kuna idadi kubwa ya watu masikini na waliotengwa katika nchi zilizoendelea pia.

2.10 Twaelewa kuwa mfumo wa sasa wa ubepari neo-huria wa kifedha husaidia matajiri na sio imara. Unachangia kuongezeka kwa kutokuwa na usawa na uporaji wa watu masikini.

2.11 Watatetea na kukuza haki za binadamu, kijamii na ya kimazingira ya watu wa rangi.

3. Mabadiliko ya hali ya hewa na Nishati

3.0 Utata wa hali ya hewa ndio changamoto kubwa zaidi inayokabili ulimwengu na vile vile nafasi kubwa kwetu binadamu kujifikiria jinsi tunavyoishi, kwa njia iliyo ya haki kijamii na inayozingatia uwezo wa ikolojia. Wanakijani wamejitolea kupunguza kuongezeka kwa joto duniani kwa kwa kiwango kisichozidi digrii 1.5 juu ya viwango vya nyakati za kabla ya viwanda.

MKATABA WA GLOBAL GREENS

Uchafuzi wa hewa duniani utahitaji kufikia kilele kabla ya mwaka wa 2020 ili tuweze kukimu kiwango cha sasa cha joto.

Wanakijani -

3.1 Wanakubaliana na lengo la kupunguza viwango vya CO2 angani hadi 450ppm katika kipindi kifupi iwezekanavyo.

3.2 Watafanya juhudi kuunga mkono mabadiliko ya haraka kufanikisha ukuzaji uchumi usiozalisha kaboni ulimwenguni kote.

3.3 Watafanya juhudi kuanzisha mfumo wa ulimwengu wa kuripoti uzalishaji wa hewa chafu kwa mashirika ya kimataifa, yaliyohusishwa na ushuru wa kaboni na uchafuzi mazingira ya kimataifa.

3.4 Watafanya bidii kuhakikisha kwamba nchi zinazoendelea zinapata teknolojia bora zaidi, endelevu na inayofaa, kwa kuzingatia kwa umakini nishati mbadala, na kwamba wanakubali kushiriki Mikutano ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa ili kuhakikisha kuwa mikataba yao inatimizwa kikamilifu ulimwenguni kote. Kanuni ya usawa lazima iwe msingi kwa majadiliano na hatua zinayohusu mabadiliko ya hali ya hewa.

3.5 Wanapinga juhudi zozote za upanuzi wa nguvu za nyuklia na watafanya juhudi kuitokomeza kwa haraka.

3.6 Wataunga mkono wito wa kusitishwa kwa juhudi mpya za utafutaji wa mafuta ya kuchimbwa

3.7. Watafanya juhudi kusitisha ukataji miti na uharibifu wa misitu kufikia mwaka wa 2020, ikizingatiwa kuwa hizo ndizo mifumo za ikolojia zilizo na kaboni nyingi zaidi duniani, ni muhimu kwa watu wa asili, ina mimea na wanyama wengi, na haiwezi ikarekebishwa upya kwa muda wa maisha ya mwanadamu.

3.8 Watakuza upandaji wa miti ya spishi tofauti lakini sio kilimo cha zao la aina moja, kama hatua ya muda mfupi ya kutega kaboni kutoka hewani, na faida zinginezo kwa mazingira.

3.9 Watahimiza utozaji ushuru kwa nishati isiyo mbadala na kuunga mkono utumiaji wa fedha zilizotolewa kukuza matumizi bora ya nishati na uimarishaji wa nishati mbadala.

3.10 Wanaunga mkono utafiti juu ya utumiaji wa vyanzo endelevu vya nishati na maendeleo ya ufundi wa uzalishaji wa nishaji kwa kuzingatia ikolojia

3.11 Wanakuza usambazaji wa teknolojia bora za nishati na miundombinu ya nguvu ya kijani kati na ndani ya nchi na soko mbalimbali bila gharama au kwa gharama ndogo. Hii ni moja ya gharama za nyakati za sasa za kiuchumi zitokanazo na uzalishaji wa hewa chafu na nchi za magharibi.

MKATABA WA GLOBAL GREENS

4. Bioanuwai

Mifumo ya mazingira yenye afya ni muhimu kwa maisha ya mwanadamu, ilhali tunaonekana kuwa tumesahau uhusiano kati ya bioanuwai na jamii. Viwango vya kutoweka kwa bioanuwai ni mara 100 hadi 1000 juu kuliko nyakati za kabla mwanadamu. Ni 20% tu ya misitu ya asili duniani isiyo na makovu yaliyosababishwa na binadamu. Asilimia 80 ya samaki tayari wamekwisha au wako katika hatari ya kwisha. Uvamizi wa mimea isiyo ya asili, wanyama na magonjwa unaenea kwa kasi. Uharibifu wa makazi na kupotea kwa spishi yanasababishwa na maendeleo ya viwanda na kilimo ambayo pia yanazidisha mabadiliko ya hali ya hewa, kutokuwa na hali ya usawa ulimwenguni na uharibifu wa tamaduni za asili na mbinu za mapato. Kilimo cha zao moja, kinachohimizwa na kilimobiashara na kuharakishwa na ukarabati wa viumbe asili na hati miliki ya viumbe, yanatishia utofauti halisi wa mimea na wanyama waliofugwa nyumbani, na kuongeza hatari ya magonjwa kuangamiza spishi hizi.

Wanakijani -

4.1 Watapinga vikali maendeleo ya kilimo na viwanda yanayosababisha uharibifu wa mazingira na kutia juhudi kimsingi kulindaji mimea na wanyama asili katika makazi yao ya asili, na inapowezekana katika maeneo makubwa.

4.2 Watafanya juhudi kuondoa ruzuku kwa shughuli zinazosababisha uharibifu wa mazingira, zikiwemo ukataji miti, unyonyaji wa mafuta ya ardhi, ujenzi wa bwawa, utafutaji madini, uhandisi wa viumbe hai na kilimo cha zao moja.

4.3 Watakuza sera za ununuzi zinazozingatia ikolojia, kwa bidhaa kama vile mbao, kwa msingi tu wa ufafanuzi wa kina zaidi wa uendelevu na unaodhibitishwa na lebo ya kuaminika.

4.4 Wanaunga mkono dhana la 'deni kwa matumizi ya mali ya asili', kulingana na makubaliano ya jamii zilizoathirika na za asili.

4.5 Watakuza urejeshaji wa mazingira asili ya yaliyoharibiwa, na usafishaji wa maeneo yenye sumu kutokana na shughuli za zamani na za sasa za kijeshi na viwanda kote ulimwenguni.

4.6 Wanazingatia kwamba kupunguza usafirishaji wa bidhaa kutoka sehemu moja hadi nyingine ulimwenguni, ikilingana na pendekezo la uzalishaji wa mahali pa matumizi inapowezekana, itakuwa na faida kuu ya kupunguza "uvamizi wa viumbehai", pamoja na kupunguza matumizi ya mafuta na uzalishaji wa gesi chafu.

4.7 Wanajitolea kukuza mtaala wa ikolojia wa ulimwengu kwa ngazi zote za elimu.

4.8 Watafanya juhudi kuanzisha mahakama ya kimataifa ya haki haswa kwa ajili ya uharibifu wa mazingira na upotezaji wa bianuwai ambapo kesi zinaweza kusikilizwa dhidi ya mashirika, mataifa, majimbo na watu binafsi.

4.9 Watakataa jambo la kuwepo na hati miliki na uuzaji wa maisha.

5. Kuongoza utandawazi wa uchumi kwa kanuni endelevu

5.0 Hamsini na tatu ya uchumi 100 kubwa ulimwenguni leo ni mashirika. Kwa kuziunganisha serikali, wameunda mfumo wa kisheria unaoweka shughuli zisizo za kiuchumi juu ya faida ya umma, hulinda ustawi wa mashirika lakini hushambulia ustawi wa jamii, na hufanya uchumi wa mataifa kutegemea kasino la kifedha la kimataifa ambalo linageuza zaidi ya $ trillion 300 kwa siku kwa shughuli za bahati na sibu. Msukosuko kwa hali ya kifedha duniani umeongeza hali tete na ukosefu wa usalama katika uchumi zote, athari kubwa zaidi ikiwa kwa watu, makundi na nchi maskini. IMF na Benki ya Dunia wamechangia kwa shida hii badala ya kusaidia kuleta suluhisho; mahitaji ya msingi wanayoegemea kwa uendeshaji shughuli zao yakiwa hayafai kwa undaji wa mfumo wa uchumi wa kimataifa, endelevu na wa haki.

Wanakijani -

5.1 Wanathibitisha kuwa vitu muhimu kwa maisha, kama vile maji, lazima vibakie kwa umiliki na udhibiti wa umma; na kwamba utamaduni, ufikiaji wa kimsingi wa chakula, afya ya kijamii na umma, elimu, na vyombo vya habari vilivyo huru sio 'bidhaa' za kufanyiwa mikataba kwa soko la kimataifa.

5.2 Waunga mkono uundaji wa Shirika la Mazingira Duniani kwa kuunganisha Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (UNEP), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP), na Kituo cha Mazingira cha Ulimwengu (GEF) kuwa taasisi moja yenye ufadhili na nguvu ya kuweka vikwazo ili kukuza maendeleo endelevu ulimwenguni. Shirika la Biashara la Ulimwengu (WTO) linapaswa kuwa chini ya maamuzi ya taasisi hii.

5.3 Waunga mkono marekebisho kwa Benki ya Dunia na IMF ili uwanachama wao na maamuzi yao yawe ya kidemokrasia, na shughuli zao zifuate kanuni za uendelevu na za mikataba yote ya kimataifa kuhusu haki za kibinadamu na za wafanyikazi, na ulinzi wa mazingira.

5.4 Wanaunga mkono marekebisho thabiti kwa WTO ili kufanya uendelevu kuwa lengo lake kuu, ikiambatana na michakato ya uwazi na ya kidemokrasia na ushiriki wa wawakilishi kutoka kwa jamii zilizoathirika. Kwa kuongezea lazima kuwe na mgawanyo wa nyadhifa ili kusitisha mfumo wa kusuluhisha mizozo kuwa wa kipekee kwa WTO. Tathmini ya athari kwa uendelevu wa mazungumzo ya awali inahitajika kabla ya hatua yoyote mpya kuchukuliwa.

5.5 Watafanya juhudi kuzuia utekelezaji wa mikataba mipya ya biashara ya kikanda au hemispheti na uwekezaji chini ya sheria za WTO, na kusaidia michakato ya ushirikianaji wa mataifa ambao utahakikisha ustawi wa watu na ubora wa mazingira.

5.6 Tutaunda mazingira ya ulimwengu ambapo taasisi za kifedha na kiuchumi na mashirika yatakuza na kulinda miradi endelevu ya mazingira ambayo itasaidia jamii katika ngazi zote (za mitaa, kikanda, kitaifa na kimataifa).

5.7 Watasisitiza kwamba makubaliano ya kimataifa juu ya mazingira, hali ya kazi na afya inapaswa kupewa kipaumbele juu ya sheria zozote za kimataifa kuhusu biashara.

5.8 Watafanya bidii kutekeleza mfumo wa Tobin-Henderson au Ushuru wa shughuli za Kifedha na vyombo vingine ili kupunguza shughuli za ubashiri wa sarafu za kimataifa na kuhimiza uwekezaji katika uchumi wa kweli, na kutenga fedha za kukuza usawa katika maendeleo ya ulimwengu.

5.9 Watafanya juhudi kuhimiza mashirika kufuata sheria za mazingira, kazi na kijamii za nchi zao na za nchi wanazofanya kazi, zile zilizo za kiwango cha juu zaidi.

5.10 Watafanya bidii kuhakikisha kwamba mashirika yote ya kimataifa, haswa ambayo yana uwezo mkubwa wa kuchangia kwa uundaji sheria za biashara ya kimataifa, yanafuata kanuni za uendelevu na yanaweka mipangilio ya mafunzo ya mabadiliko ya kitamaduni ili kutimiza lengo hili kikamilifu.

5.11 Wanataka ustawi wa ushirika kufanywa wazi na wenye kiwango sawa cha uwajibikaji kama ustawi wa jamii, na ruzuku kwa shughuli zinazosababisha uharibifu kwa mazingira na jamii zikomeshwe kabisa.

5.12 Wanasasisha maendeleo ya ujasiriamali kwa raia ili kukuza uchumi kwa kijamii kama njia ya kupambana na kutengwa kwa kijamii kunakosababishwa na utandawazi wa uchumi

6. Haki za binadamu

6.0 Kukataliwa kwa haki za binadamu na uhuru huambatana na umaskini na ukosefu wa nguvu ya kisiasa. Mamilioni huathirika kwa ubaguzi, vitisho, kuzuiliwa bila sababu, vurugu na kifo. Robo tatu ya serikali za ulimwengu zimetumia mateso katika miaka mitatu iliyopita.

Wanakijani -

6.1 Wanaunga mkono Azimio la Ulimwenguni la Haki za Binadamu, Agano la Kimataifa juu ya Haki za Uchumi, Jamii na Utamaduni, Agano la Kimataifa juu ya Haki za Kiraia na Siasa, mikataba ya Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO), na vyombo vingine vya kimataifa vinavyolinda haki na uhuru. Tunaamini kwamba haki hizi ni za watu wote ulimwenguni na haziwezi kugawanywa na kwamba serikali za kitaifa zina wajibu wa kuzitekeleza.

6.2 Wanalaani udikteta wote na serikali zinazokiuka haki za binadamu, bila kujali madai yao ya kisiasa

6.3 Watashirikiana na jamii mitaani kukuza uhamasishaji wa haki za binadamu, na kuhakikisha kuwa Tume ya UN ya Haki za Binadamu na mashirika mengine kwa huo mkataba yana rasilimali za kutosha.

6.4 Wanatoa wito wa Azimio la ulimwengu la Haki za Binadamu kurekebishwa ili kujumuisha haki ya kuwa na mazingira mazuri na haki ya vizazi vyote kwa maliasili na ya kiutamaduni.

6.5 Wanazingatia haki ya wanawake kufanya maamuzi yao, ikiwa ni pamoja na kudhibiti uzazi wao kwa njia wanayoona inafaa bila ubaguzi au kutumia nguvu, kuunga mkono Muungano wa Kutokomeza Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW), wanahimiza ambao hawajaidhinisha kwa kutia saini kifanya hivyo na kuridhia bila kuchelewesha zaidi na kuwahimiza walioidhinisha tayari kuviondoa vikwazo vyote.

6.6 Waunga mkono haki ya watu asilia kujitawala, kumiliki ardhi, na kuwa wa haki za jadi za uwindaji na uvuvi kwa ajili ya kujikimu, kwa kutumia mbinu za kibinadamu na za uendelevu kwa ikolojia; na kuunga mkono hoja za watu asilia kuanzisha na kufanya kazi kupitia miungano yao ya kimataifa.

6.7 Wanaunga mkono Azimio la UN juu ya haki za watu asilia kama kiwango cha chini cha ulinzi kinachokubaliwa na watu wa kiasili, na hatua za watu asilia kuanzisha na kufanya kazi kupitia miungano yao ya kimataifa.

6.8 Wanashurutisha ya kuwa wanyanyasaji wawajibike, na watafanya harakati ili wahukumiwe, katika nchi zao au mahali pengine, mbele ya jopo la kimataifa la majaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai.

6.9 Wanapinga ukiukaji wowote wa uadilifu wa mwili wa binadamu kwa kuteswa, adhabu au mienendo mingine yoyote ikiwa ni pamoja na ukeketaji wa kitamaduni na wa kidini.

6.10 Wanatoa mwito wa kusitishwa kwa adhabu ya kifo ulimwenguni kote.

6.11 Wanatoa wito kwa serikali kuhakikisha kuwa wote wanaotafuta hifadhi, iwe ni waathiriwa wa vurugu za serikali au vikundi vingine vyenye silaha, wanashughulikiwa kulingana na Mkataba wa Geneva wa 1951 wa Haki za ukimbizi; wanapata huduma kwa haki; hawazuiliwi kiholela; na hawarudishwi katika nchi ambayo wanaweza athirika kwa ukiukaji wa haki zao za msingi za kibinadamu, au kukabiliwa na hatari ya kifo, mateso, au unyanyasaji mwingine wa kinyama.

6.12 Wanatoa wito wa kupiga marufuku kufukuzwa kwa pamoja.

6.13 Wanazingatia haki ya wafanyikazi wote kupata kazi salama, inayolipwa vizuri, na uhuru wa wao kuunda muungana.

6.14 Wanaunga mkono haki ya watoto ya kukua huru bila hitaji la kufanya kazi, na kuanzishwa kwa udhibiti wa kiumri wa kuruhusu watoto kushirikishwa kikazi.

6.15 Wanadai kuhalalishwa kwa mahusiano ya kimapenzi ya jinsia moja, kutambulika kisheria kwa mahuntha na watu wa jinsia iliyokandamizwa, ulinzi wa haki ya uhuru wa mwili ikiwa ni pamoja na kwa watu wa jinsia mbili, na haki sawa kwa uhusiano wa jinsia moja.

Wanashikilia kanuni kwamba kila mtu ana haki ya kupenda na kuanzisha familia. Tunaunga mkono jamii mitaani katika wito wao wa usawa wa ndoa au aina nyingine yoyote ya familia au ushirikiano ambao wanaona unafaa kwa muktadha wao.

Kupitia mashirika yao ya uwanachama, watashinikiza serikali kukomesha adhabu yoyote, dhuluma na unyanyasaji dhidi ya watu wa LGBT+ na kutekeleza kanuni za Yogyakarta juu ya Utumiaji wa Sheria ya Haki za Binadamu ya Kimataifa kuhusiana na utofauti wa kijinsia na utambulishaji wa jinsia.

Tunaomba serikali zote ulimwenguni ziondoe sheria ambazo zinaona mwelekeo wa kijinsia na tabia za LGBTIQ + kama sio halali. Jamii za LGBTIQ + hazipaswi kunyimwa kisheria haki zao za mali, uhuru wa kibinafsi, na maisha kwa sababu ya mwelekeo wao wa kijinsia na tabia.

Tunapinga serikali yoyote ambayo inapiga marufuku, kuzuia, au kukandamiza habari za LGBTIQ, + hotuba, kazi, na mipango mingine, na kushiriki ubaguzi.

Tunahitaji kwamba utangulizi wa maswala ya LGBTIQ + uanzishwe katika kila ngazi ya serikali. Mashirika yote wa serikali lazima, wakati wa kuunda, kutekeleza na kutathmini aina zote za sera na huduma, kuzingatia hali, mahitaji, na athari kwa jamii ya LGBTIQ +. Wanapaswa kuzingatia kwa uangalifu ikiwa rasilimali zinatosha na kushughulikia jambo la ubaguzi. Kuhakikisha ufanisi, jambo la utangulizi wa maswala ya LGBTIQ + linapaswa kupangwa na kuratibiwa na shirika lililoteuliwa kwa kiwango cha juu.

6.16 Watafanya juhudi kuboresha fursa za walemavu kuishi na kufanya kazi kwa usawa katika jamii, pamoja na ushiriki wa kweli wa kisiasa.

6.17 Wanaunga mkono haki ya wachache kilugha kuitumia lugha yao wenyewe.

7. Vyakula na Maji

7.0 Mamia ya mamilioni ya watu wanabakia kuwa na afya mbaya, sio kwa sababu ya ukosefu wa chakula cha kutosha bali kwa sababu ya kutokuwepo kwa uwezo sawa wa kupata ardhi, maji, mkopo na masoko kwa watu wote. Viumbe vilivyobadilishwa kwa vinasaba (GMOs) sio suluhisho, kwa sababu tatizo la dharura sio uzalishaji bali ni usambazaji. Zaidi ya hayo, GMOs zinahatarisha hali ya mazingira, wakulima wadogo wanaojitegemea, watumiaji, na viumbe hai

ambavyo ni bima yetu bora dhidi ya maafa kwa kilimo. Uhaba wa maji unatishia katika vyanzo vya juu ya ardhi na pia vya chini ya mchanga. Ukataji miti kwa misitu unasababisha maporomoko ya ardhi na mafuriko, na majangwa pamoja na uharibifu wa mazingira kuenea zaidi. Jambo moja la afueni ni vile kilimo kisichotumia kemikali kinavyoimarika kwa kasi.

Wanakijani -

7.1 Wanaamini kuwa upatikanaji wa maji safi kwa mahitaji ya msingi ni haki ya kimsingi na kupinga ubinafsishaji wa rasilimali za maji na miundombinu.

7.2 Watafanya juhudi kuondoa ruzuku ya maji, kando na ruzuku ya kijamii, na kufanya matumizi ya maji kuwa bora zaidi.

7.3 Watafanya bidii kuhakikisha kuwa maji safi ya mito na iliyopo chini ya ardhi inahifadhiwa kwa ubora na wingi na imewekewa bei ipasavyo kuhakikisha rasilimali hizi zinalindwa vya kutosha ili zisipungue.

7.4 Wanaamini kuwa uimara wa eneo za chemichemi na afya ya mifumo ya mito ni muhimu, na watafanya kazi na watu walioathirika moja kwa moja kumaliza uharibifu wa mito, ikiwemo mabwawa mapya na miradi ya umwagiliaji, na ukataji wa miti kwa chemichemi.

7.5 Tutafanya kazi na jamii mitaani katika maeneo kame, ambako hali ya hewa haitabiriki kwa uhakika, ili kupunguza uharibifu wa ardhi.

7.6 Wanazijali nchi ambazo zimeathiriwa sana na hali ya jangwa na ukataji miti, na kuuliza nchi ambazo bado hazijaridhia Mkataba wa UN wa Uenezi wa Jangwa kufanya hivyo, na kutengwe rasilimali zinazostahiki kutimiza mkataba huu.

7.7 Wataunga mkono na kukuza kilimo kisichotumia kemikali.

7.8 Wanatoa mwito wa kupiga marufuku ukuzaji wa kibiashara wa mazao yaliyobadilishwa vinasaba ulimwenguni kote.

7.9 Watafanya juhudi kuhakikisha kuwa chakula kiko salama, na kanuni kali kwa uzalishaji, uhifadhi na uuzaji.

7.10 Watafanya juhudi kuhakikisha kuwa utafiti wa kisayansi unafanywa kwa maadili na kutumika kulingana na kanuni za tahadhari.

7.11 Wanatoa mwito kwa kuondolewa kwa kemikali zote zilizotengenezwa na binadamu zinazokawia na kujilimbikiza kwa mazingira na kutia jitihada kuondoa kemikali zote hatari kwa mazingira.

7.12 Watafanya bidii kuhakikisha kuwa homoni za kuimarisha ukuaji wa wanyama zimepigwa marufuku, na kanuni kali za kutawala matumizi ya dawa za kutibu magonjwa kwa wanyama zinatekelezwa.

7.13 Watafanya juhudi kuhakikisha wanyama wote wanaangaliwa kwa njia isiyo ya ukatili wakati wa uzalishaji, usafirishaji na kuchinjwa na watahakikisha ustawi wa wanyama.

7.14 Watafanya bidii kuhakikisha kuwa athari za mmomomyoko, mafuriko na athari zingine za kimazingira zinarekebishwa na kwamba hatua mwafaka za urekebishaji zinatekelezwa.

8. Mipango Endelevu

Matumizi katika nchi zilizoendelea ni ya kupindukia kwa kipimo chochote kile, na kwa kiasi kikubwa ndichi chanzo cha kupungua kwa ubora wa mazingira. Nchi mpya zinazoendelea pia zinaongeza matumizi yao, ambayo itaongeza sana kwa shinikizo la ikolojia. Tunapozingatia uchumi wa kijani - unaoiga michakato ya ikolojia, kupunguza taka kwa kutumia kwa njia mbadala na kuunda upya bidhaa zilivyotumika, na kusisitiza shughuli zinazoongeza ubora wa maisha na uhusiano badala ya utumiaji wa bidhaa - huleta ahadi ya ajira mpya, viwanda vyenye uchafuzi mdogo, mazingira bora ya kazi na maisha ya hali ya juu.

Wanakijani -

8.1 Wanahimiza utumizi wa hatua za ustawi badala ya Pato la Taifa kupima maendeleo, na kutambua mipaka ya ikolojia kwa ukuaji wa nyenzo na matumizi.

8.2 Wanaelewa kuwa raia wa nchi zilizoathiriwa na mradi wa maendeleo wana haki ya kushiriki katika maamuzi juu yake, bila kujali mipaka ya kitaifa.

8.3 Watafanya juhudi kuhakikisha kuwa wale wanaonufaika kwa kutumia rasilimali yoyote ya umma na/au asili wanapaswa kulipa kodi kamili kwa bei la soko kwa matumizi ya rasilimali hizi, na kwa uharibifu wowote wanaofanya kwa rasilimali nyingine yoyote ya umma.

8.4 Wanatambua kuwa athari ya ukuaji wa miji kwenye ardhi ya kilimo na mazingira ya asili lazima iwe na mwelekeo na mwishowe ikomeshwe.

8.5 Wanatambua kuwa mchakato wa uhamiaji mijini kutokana na umaskini vijijini lazima upunguzwe na kufanyiwa urejesho kupitia programu mwafaka za maendeleo vijijini ambazo zinalinda mienendo na mazingira ya makaazi ya vijijini.

8.6 Inaunga mipango ya mitaani ya biashara endelevu kiikolojia, makaazi, usafiri, usimamizi wa taka, mbuga, misitu ya jiji, nafasi za umma; na itaanzisha mahusiano kati ya Wanakijani katika ngazi ya kawaida na ya kikanda ulimwenguni kote ili wabadilishane habari na kusaidiana.

8.7 Watafanya bidii kupunguza uchafuzi wa mazingira ya mjini kwa unaosababishawa na magari kwa kupinga upanuzi kila uchao wa idadi ya barabara zinazotumika bila malipo; kuhimiza utumiaji wa magari yatumiayo nishati kidogo; kusanifisha upangaji wa matumizi ya ardhi na usafiri wa umma, uendeshaji baiskeli na kutembea; kupea kipaumbele mipango ya usafirishaji ya watu wengi dhidi ya ufadhili kwa miundombinu ya magari ya kibinafsi; na kutupilia mbali sera za ushuru zinazopendelea maendeleo ya watu binafsi.

8.8 Watashughulikia kuunda mikakati ya kiuchumi ya uwajibikaji kwa jamii, kutumia ushuru na fedha za umma kuongeza motisha kwa usambazaji wa mali kwa haki, na kodi ya kiikolojia ili kutoa motisha ya kuzuia taka na uchafuzi wa mazingira.

8.9 Watahitaji mashirika na jamii kupunguza, kutumia tena na kuchakata taka, kwa lengo la kuafikia uchumi usio na taka ambao unaiga mfumo wa mazingira asili.

8.10 Wataunga mkono sera zote zinazoruhusu nchi kuongeza uvumbuzi wa kazi kupitia shughuli za kiuchumi zinazoongeza thamani, au kupitia kuchakata tena rasilimali, utengenezaji wa bidhaa zinazodumu, kilimo kisichotumia kemikali, nishati mbadala na ulinzi wa mazingira.

8.11 Wanakuza uwekezaji unaowajibika kijamii na uuzaji wa ikolojia ili wateja waweze kufanya maamuzi mwafaka kwa msingi wa taarifa za kuaminika.

8.12 Wanatambua thamani ya maarifa na imani za jadi na za mashinani, na kuunga mkono utumizi wake katika mipango na miradi.

9. Amani na Usalama

9.0 Tunaelewa amani kuwa zaidi ya ukosefu wa vita. Jitihada za kuleta amani ndio msingi wa ajenda ya Kijani kila wakati. Sababu za migogoro zinabadilika. Athari za mabadiliko ya hali ya hewa, ushindani wa maji, chakula na rasilimali yatazidi kuwa muhimu. Utofauti kati ya vita, uhalifu uliopangwa na unyanyasaji mkubwa wa haki za binadamu unazidi kuwa mgumu kutathmini. Tangu mwaka wa 2001 'vita dhidi ya' ugaidi 'pia vimesababisha ukiukaji wa haki za binadamu kwa kudanganyishia uimarishaji wa usalama. Biashara ya silaha inakua na kuenea ulimwenguni, ikinogeshwa na ukosefu wa sheria za WTO dhidi ya ruzuku. Kama shirika la ulimwengu, tunalo jukumu muhimu la kuimarisha uhusiano kati ya mashirika ya jamii yanayofanya kazi kuimarisha haki za binadamu na amani, na kusaidia na kuchagiza kwa dhana zinazoibuka na taasisi za utawala wa ulimwengu.

Wanakijani -

9.1 Wanaunga mkono jukumu la kuimarisha Umoja wa Mataifa kama shirika la kimataifa la usimamizi wa migogoro na kulinda amani, tukizingatia kuwa, ambapo kuzuia kunashindwa na katika hali ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na/au mauaji ya halaiki, utumiaji wa

nguvu unaweza kuidhinishwa ikiwa ndio njia ya pekee ya kuzuia ukiukwaji zaidi wa haki za binadamu na mateso, mradi inatumiwa chini ya agizo la Umoja wa Mataifa. Hata hivyo, nchi yoyote ina haki ya kutounga mkono au kushirikiana na hatua hiyo.

9.2 Watafanya kampeni kwa ajili ya kuongezewa nguvu zaidi nchi za Kusini katika Umoja wa Mataifa, kukomesha uturufu katika Baraza la Usalama, kuondoa kikundi cha uwanachama wa kudumu, na kuongeza idadi ya mataifa shirika.

9.3 Twaunga mkono Korti ya Makosa ya Jinai. Katika uhalifu wa kivita, unyanyasaji wa kijinsia kama vile ubakaji wa halaiki unapaswa kuzingatiwa kama uhalifu wa kivita, na vile vile uhalifu wa mazingira unaotokea wakati wa migogoro.

9.4 Wanatia jitihada kupunguza nguvu ya ushirikiano wa kijeshi-viwanda-kifedha ili kupunguza kabisa biashara ya silaha, kuhakikisha uwazi wa utengenezaji bidhaa na kuondoa ruzuku fiche zinazonufaisha tasnia ya kijeshi.

9.5 Watafanya kazi kudhibiti na kupunguza, kwa madhumuni ya kumaliza hatimaye, biashara ya silaha ya kimataifa (pamoja na kupiga marufuku silaha za nyuklia, kibaolojia na kemikali, silaha za urani na mabomu ya migodi) na kuziweka chiniya udhibiti wa Umoja wa Mataifa.

9.6 Watasaidia kuimarisha mipango iliyopo ya amani na kuanzisha mipango mipya ambayo itashughulikia masuala yote ya kuimarisha uendelezaji wa amani. Mipango zitajumuisha uchambuzi wa vyanzo vya vurugu, pamoja na vurugu za ndani ya familia, na suala la kuheshimiana baina ya jinsia; na kusaidia kupeana mafunzo ya utatuzi wa migogoro isiyo ya vurugu katika kila ngazi.

9.7 Wanaazimia kurekebisha sheria za kimataifa za ushirikishi wa kijeshi ili kuhakikisha kuwa maliasili zinalindwa vya kutosha katika mizozo.

9.8 Tutapinga mradi wowote wa Kombora la Ulinzi Taifa, na kuhakikisha kusitisha shughuli za uimarishaji wa jeshi na vifaa vya nyuklia.

10. Utendakazi wa Kimataifa

10.0 Global Greens ni mashirika huru kutoka kwa tamaduni na asili mbalimbali wanaoshiriki nia moja na kutambua kwamba, ili kuifanikisha, lazima tuchukue hatua kimataifa na pia ndani ya nchi.

Wanakijani -

10.1 Watafanya kazi kwa ushirikiano ili kutekeleza Mkataba wa Global Greens kwa kuchukua hatua kwa pamoja juu ya maswala yanayoathiri ulimwengu kila inapohitajika.

10.2 Watapiga jeki uanzilishi wa vyama vya Kijani, harakati za kisiasa na ushirikiano wa vijana ulimwenguni kote.

10.3 Watasaidia, kwa maombi yao, vyama vingine na harakati za Kijani ikiwemo kwa - kutoa wachunguzi wa kiuchaguzi kusaidia kuhakikisha kuwa ni za huru na haki; - kuhimiza wapiga kura kujiandikisha na kupigia kura vyama vya Kijani katika nchi zao.

10.4 Tutapitisha na kutekeleza katika mashirika yetu kanuni za kidemokrasia tunazotafuta katika jamii.

10.5 Tutakua kielelezo cha demokrasia shirikishi ndani ya shirika letu lenyewe katika ngazi zote.

10.6 Tutahimiza ushirikiano kati ya vyama vya Kijani ulimwenguni kuhakikisha kuwa vyama shiriki vinashauriwa, kuelimishwa na vina uwezo sawa wa ushawishi kwa nafasi za wanakijani ulimwenguni.

10.7 Tutahimiza vyama na harakati za kisiasa za Kijani kuonyesha uongozi katika kubuni sera zinazohakikisha uwazi na ugatuzi, ili nguvu ya kisiasa na fursa iwe kwa wanachama wote; na katika kutengeneza miundo mpya za kisiasa ambazo zinakabiliana vyema na changamoto za maendeleo endelevu na demokrasia mashinani.

10.8 Tutaepuka vyanzo vya fedha ambavyo vinatofautiana na maono na maadili yetu.

10.9 Tutaepuka kushirikiana na udikteta, madhehebu, au mashirika ya jinai na yale yanayoyategemea, haswa katika maswala ya demokrasia na haki za binadamu.

10.10 Tutaimarisha ushirikiano wetu na mashirika ya kijamii yaliyo na nia ziambatanazo na zetu, na mashirika za asasi ya uraia; sisi ni sehemu moja, pamoja nao, kwa ufahamu unaoendelea kuimarika kwamba heshima kwa mazingira, kwa haki za kijamii na kibinadamu, na kwa demokrasia, lazima yawepo kwa shirika la kiuchumi la ulimwengu.

10.11 Tutasaidiana kibinafsi na kisiasa kwa urafiki, matumaini na kwa furaha, bila kusahau kujifurahisha katika mchakato huo!